

Shairi lifuatalo liliandikwa na Malenga Hamidu Tambwe miaka kadha iliyopita likizungumzia umuhimu wa utunzi mzuri wa mashairi na nasaha za kimaisha

HIFADHI JAPO KIBOVU

1. Sikiza nikuambie, usije kushika shavu,
La kufanya usijue, mithili ya mpumbavu,
Ni mema yazingatie, tena shitadi kwa nguvu,
Hifadhi japo kibovu, kitu kilichotumiwa.
2. Usitupe jalalani, japo kwa fedha mpevu,
Ni kunga ya duniani, iko siku ya utovu,
Utajikuta tabani, wabaki kukuna ndevu,
Hifadhi japo kibovu, kitu kilichotumiwa.
3. Tamthili ya kizima, kikawa ni kilegevu,
Ikawa sasa ni chema, kilichoitwa kibovu,
Yaani chenyewe chema, ijapo hakina nguvu,
Hifadhi japo kibovu, kitu kilichotumiwa.
4. Hali ya namna hiyo, tapata ukakamavu,
Kitajimudi ndondoo, na wake ubovu bovu,
Ela muda kama huo, waenda pasi maovu,
Hifadhi japo kibovu, kitu kilichotumiwa.
5. Haya kwa bahati mbaya, ulijipa ushupavu,
Kibovu kujitupiya, leo katu huna nguvu,
Aibu itakujiya, ukiomba kwa wapevu,
Hifadhi japo kibovu, kitu kilichotumiwa.
6. Mithili yake makombo, ya wali na ndizi mbivu,
Ambayo sasa ni shombo, huliwa na walegevu,
Yafunikize kwa chombo, bila ya uchelewevu,
Hifadhi japo kibovu, kitu kilichotumiwa.
7. Haya kesho wala wali, kwa kiteweo cha ndovu,
Umeula na umbali, bado kuujaza wavu,
Halafu huna wa pili, utajaza kwa mbovu,
Hifadhi japo kibovu, kitu kilichotumiwa.
8. Ungeyatupa makombo, ungekuwa nayo mavu,
Ukawa hutendi jambo, kwa kuwa umlegevu,
Kwa hiyo huna misimbo, ni rijali mwenye nguvu,
Hifadhi japo kibovu, kitu kilichotumiwa.
9. Kama nimeamba mema, shika kwa ukakamavu,
Penye kosa weka jema, jema lisilo na ovu,
Kisha ubaki tundama, uitwe mvumilivu,
Hifadhi japo kibovu, kitu kilichotumiwa.
10. Alhamdulillah, siongezi neno ovu,
Yangu yote nimewahi, kuyapanga kama mbavu,
Kwa hiyo utanabahi, kuepuka upotovu,
Hifadhi japo kibovu, kitu kilichotumiwa.

Hamidu R. Tambwe (1967)